TMA
TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY
MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

*Na.15: Msimu wa Kilimo 2025/26* *Tathmini ya Februari 21 -28, 2026 na Matazamio kwa Kipindi cha Machi 1-10, 2026*

**MUHTASARI**

- Mvua zinazotarajiwa katika maeneo mengi nchini, zitasaidia katika ukuaji wa mazao.
- Wakulima katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka wanashuriwa kumalizia shughuli za uandaaji wa mashamba na kuendeleaa na upandaji wa mazao kwa ajili ya msimu wa mvua za masika.
- Wakulima na wadau wa kilimo wanashauriwa kushirikiana na maafisa ugani katika maeneo yao huku wakiendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa kwa mipango thabiti ya shughuli za kilimo.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 21-28, 2026

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kupungua nguvu wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika. Hali hii ilidumisha mwenendo wa ukandamvua (ITCZ) katika maeneo ya magharibi mwa nchi, kanda ya Ziwa Victoria, nyanda za juu kusini magharibi na kusini mwa nchi. Kwa upande mwingine joto la bahari katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi lilikuwa la wastani hadi chini ya wastani. Hali hii ilipelekea kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani na maeneo jirani.


Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea uwepo wa vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria, kanda ya kati, kusini mwa nchi, nyanda za juu kaskazini mashariki, pwani ya kaskazini, nyanda za juu kusini magharibi na magharibi.

## TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 21-28, 2026

Katika dikadi, maeneo mengi nchini yalipata kiasi cha mvua cha siku kumi kati ya milimita 50 na 100, hali inayoonesha uwepo wa mvua za wastani zilizosambaa katika sehemu kubwa ya nchi.

Kiasi cha juu zaidi cha mvua kati ya milimita 200 na 250, kimerekodiwa katika maeneo ya kaskazini mwa mkoa wa Morogoro.

Kwa upande mwingine, kiasi cha mvua cha chini ya milimita 50, kimerekodiwa katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Kigoma, Kagera, Geita, Shinyanga, Rukwa, Mtwara, Lindi na Tabora kama inavyoonekana katika Kielelezo cha 1.




Kielelezo 1: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Februari 21-28, 2026

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 21-28, 2026

Katika dekadi hii, kiasi cha mvua kilichorekodiwa katika maeneo mengi nchini kimesaidia kuongeza unyevunyevu wa udongo, hali ambayo imesaidia katika ukuaji wa wa mazao.

Katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka, hususan ukanda wa Pwani ya Kaskazini, Bonde la Ziwa Victoria pamoja na baadhi ya maeneo ya nyanda za juu kaskazini-mashariki, wakulima wengi wanaendelea na upandaji wa mahindi na maharagwe huku wachache wakikamilisha maandalizi ya mashamba. Unyeshaji wa mvua unaendelea kuwa mzuri na unasaidia katika ukuaji wa mazao.

Kwa mkoa wa Morogoro, zao la mpunga liko katika hatua ya kutoa machipukizi. Ongezeko la mvua lililojitokeza linaweza kuimarisha ukuaji wa mpunga, hususan katika mashamba yanayotegemea mvua.

Katika maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka, mahindi yako katika hatua ya ukuaji, ingawa katika mkoa wa Tabora mahindi yamefikia hatua ya kubumba. Katika mkoa wa Dodoma, mazao ya alizeti na mtama yako katika hatua za awali za ukuaji.

Mazao ya kudumu kama kahawa, hususan katika mikoa ya Kilimanjaro na Songwe, yako katika hatua ya kutunga matunda. Uwepo wa unyevunyevu wa kutosha kwenye udongo umeendelea kusaidia ukuaji wa kahawa katika hatua hii.

Upatikanaji wa maji na malisho kwa mifugo na wanyamapori umeongezeka kiasi katika maeneo yaliyopata ongezeko la mvua.

## HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 21-28, 2026

Kwa ujumla kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito viliongezeka kiasi kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha katik maeneo mbalimbali nchini.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 1-10, 2026

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kuimarika kuliko ile iliyopo kusini mwa dunia. Hali hii inatarajiwa kusababisha uwepo wa ukandamvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi, Kanda ya Ziwa Victoria, nyanda za juu kusini magharibi na kusini mwa nchi. Kwa upande mwingine joto la bahari katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la wastani hadi Juu ya wastani wakati joto la bahari katika eneo la mashariki mwa Bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la Wastani hadi Chini ya Wastani. Hali hii inatarajiwa kupelekea upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka baharini kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani ya nchi na yale ya nyanda za juu kaskazini mashariki na hivyo kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 1-10, 2026

Maeneo ya kanda ya ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) na Nyanda za juu kaskazini-mashariki yanatarajia kupata vipindi vifupi vya mvua kubwa zinazoambatana na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo hususan katika kipindi cha siku tano za mwanzo wa dikadi.

Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) na kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida) yanatarajiwa kupata vipindi vya mvua zinazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache.

Magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) na nyanda za juu kusini-magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) yanatarajiwa kupata mvua zinazoambatana na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo.

Pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) na kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro) yanatarajia kupata vipindi vya mvua zinazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache.

## HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA MACHI 1-10, 2026

Hali ya mvua inayotarajiwa katika maeneo mengi nchini itaongeza unyevu nyevu katika udongo na kusaidia ukuaji wa mazao.

**Ushauri:**

- **Maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua (kanda ya ziwa Victoria, Pwani ya Kaskazini na Nyanda za juu Kaskazini Mashariki):** Hali ya mvua zinazoambatana na ngurumo za radi inayotarajiwa itasaidia katika shughuli za uandaaji wa mashamba kwa msimu wa kilimo wa Masika unaotarajiwa**.**
- **Maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua (nyanda za juu kusini magharibi, mikoa ya magharibi, Pwani ya kusini na Kanda ya kusini):** Mvua zinazotarajiwa katika maeneo haya zitasaidia ukuaji wa mazao.
- Wakulima katika maeneo haya wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku kwa mipango thabiti ya shughuli za kilimo.
- **Malisho na upatikanaji wa maji kwa wafugaji:** Wafugaji wanashauriwa kupanda majani ya malisho na kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadae.
- **Wavuvi wa Samaki baharini na maziwa makuu:** Wavuvi wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku ili kujua wakati sahihi wa kufanya shughuli za uvuvi kutokana na uwezekano wa kujitokeza mawimbi makubwa na upepo mkali

## HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 1-10, 2026

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuendelea kudumishwa kutokana na hali ya mvua inayotarajiwa.

Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, Chuo Kikuu cha Dodoma,
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz; agromet@meteo.go.tz; Tovuti: *www.meteo.go.tz*
(ISO 9001:2015 Certified in Aviation Services)